# UCHUMI & BIASHARA u&b

## 'Umeme, barabara na maji vinahitaji mpango mkakati'

**Na Grace Ndossa**

NISHATI ya umeme, barabara, na maji vinahitaji mpango mkakati wa muda mrefu, uwekezaji mkubwa wa sekta za umma na sekta binafsi zenye dhamira ya dhati ya kutekeleza miradi iliyopangwa.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa CTI Bi.Christine Kilindu wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa wachoraji katuni za mazingira ya biashara yaliyofanyika hivi karibuni.

Alisema mwaka 2000, CTI iliandaa ripoti kuhusu mfumo wa sheria na kanuni ambazo iliainisha sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na biashara. Baadhi ya sheria na kanuni hizo zilikuwa zinapingana, na hivyo kuwachanganya wale wenye jukumu la kuzifuata au kuzitumia.

Alisema Ripoti ya Mitazamo ya Viongozi wa Biashara ambayo ilitolewa kwa lengo mahsusi la kuchukua maoni ya jumuiya za biashara za Tanzania pia ugumu uliopo wa kufanya biashara nchini, na miongoni mwa changamoto zilizoainishwa ambazo ndizo zimeonekana kuwa kero kubwa katika kukwamisha uendeshaji biashara.

"Tumeungana na mashirika mengine mawili ya biashara: Shirikisho la Utalii la Tanzania (TCT) na VIBINDO, ambao ndio marafiki na washirika wetu katika suala zima la utetezi wa mazingira bora ya biashara. Tunaweza kuwakilisha majimbo tofauti, lakini lengo letu ni moja, tunataka majimbo yetu yaweze kufanya biashara zao kwa urahisi na kwa gharama nafuu,"alisema

USAJILI



**Na Peter Twite**

BENKI ya CRDB imetoa zaidi ya sh. milioni 60 kwa ajili ya kuchangia harambee ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini kinachotarajiwa kujengwa katika Dayosisi ya Kanda ya Nyanda za Juu.

Mchango huo ulikabidhiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Dkt. Charles Kimei,wakati wa ibada maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya kuchangia ujenzi huo iliyofanyika Mbeya.

Akizungumza katika hotuba yake wakati wa ibada hiyo, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri, (KKKT) Dayosisi ya Kusini Njombe, Bw.Isaya Mengele aliwataka viongozi nchini kutenda haki, uzalendo na kuacha ubinafsi kwa jamii ili kutokomeza ufisadi unaolitikisa taifa la Tanzania.